



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UCHAGUZI MDOGO WA
MADIWANI KATIKA KATA 14 TANZANIA BARA

Dodoma, 14 Juni, 2023

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa, akiitarifu Tume kuhusu uwepo wa nafasi wazi za Madiwani katika Kata 14 za Tanzania Bara. Waziri ametoa taarifa hiyo kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

Kutokana na taarifa hiyo, Tume kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, inatoa taarifa kwa Umma kuhusu uwepo wa uchaguzi mdogo wa madiwani katika kata 14 za Tanzania Bara.


Kata zinazohusika na uchaguzi huo mdogo ni kutoka halmashauri 13 zilizopo katika mikoa tisa kama ifuatavyo; -

NA	MKOA	NA	HALMASHAURI	KATA
1.	TABORA	1	Wilaya ya Sikonge	Ngoywa
		2	Wilaya ya Uyui	Kalola
2.	TANGA	3	Wilaya ya Handeni	Sinden
		4	Wilaya ya Muheza	Potwe
		5	Wilaya ya Korogwe	Kwashemshi
		6	Wilaya ya Mkinga	Bosha

NA	MKOA	NA	HALMASHAURI	KATA
3.	PWANI	7	Wilaya ya Kibiti	Mahege
4.	SIMIYU	8	Mji wa Bariadi	Bunamhala
5.	KILIMANJARO	9	Wilaya ya Same	Njoro
				Kalemawe
6.	MTWARA	10	Wilaya ya Masasi	Mnavira
7.	NJOMBE	11	Wilaya ya Makete	Kinyika
8.	MOROGORO	12	Wilaya ya Kilosa	Magubike
9.	KATAVI	13	Wilaya ya Mpimbwe	Mbede

Kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi mdogo iliyotolewa na Tume, zoezi la utoaji wa fomu litafanyika kuanzia tarehe 24 hadi 30 Juni, 2023, uteuzi wa wagombea katika uchaguzi huo utafanyika tarehe 30 Juni, 2023, kampeni zitafanyika tarehe 01 hadi 12 Julai, 2023 na siku ya uchaguzi itakuwa tarehe 13 Julai, 2023.

Tume inatumia nafasi hii kuvikumbusha vyama vya siasa, wagombea na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi, Taratibu, Miongozo na maelekezo katika kipindi cha uchaguzi huu mdogo.



Kailima, R. K
MKURUGENZI WA UCHAGUZI